



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA MBINGA



Unapojibu tafadhali taja:

Kumb.Na. MDC/I.20/21/09

Tarehe: 31 Oktoba, 2023

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI AJIRA YA MKATABA

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga anapenda kuwatangazia nafasi za ajira ya mkataba kwa wa mienzi mitatu kwa Watanzania wenye sifa kama ifuatavyo:-

Nafasi inayotangazwa ni:-

1. MKUSANYA USHURU (Nafasi Moja)

i. SIFA ZA MWOMBAJI:

- ✓ Mwombaji lazima awe raia wa Tanzania na awe tayari kufanya kazi katika Kijiji/Kata na sehemu yoyote ambayo kuna vyanzo vya mapato.
- ✓ Awe na akili na muaminifu.
- ✓ Awe na kitambulisho cha Taifa (NIDA)
- ✓ Muombaji awe na umri usiopungua miaka 18 na usiozidi miaka 45.
- ✓ Awe na uwezo wa kutumia simu janja/POS.
- ✓ Muombaji aambatanishe maelezo binafsi (CV)
- ✓ Muombaji ambatanishe nakala za vyeti ya taaluma. Cheti cha kidato cha nne/sita, cheti cha kuzaliwa na picha za rangi za hivi karibuni na ziandikwe majina kwa nyuma. Nakala hizo zithibitishwe na hakimu au Wakili.
- ✓ Awe na wadhamini wa 3 wenye mali zisizo hamishika.
- ✓ Asiwe mwajiriwa wa Serikali.
- ✓ Awe anaishi jirani na Ofisi ya Halmashauri ya Wilaya Mbinga (Kiamili)

ii. KAZI NA MAJUKUMU:

- I. Kukusanya mapato katika kituo atakachopangiwa.
- II. Kutunza kumbukumbu za risiti atakazo benki makusanyo ya siku husika na .
- III. Kutunza vizuri mashine ya kukusanya mapato (POS) na vifaa vingine atakavyokuta mahali pakufanyia kazi.
- IV. Kuwasilisha makusanyo katika akaunti ya Halmashauri .
- V. Kufanya kazi zote atakazopangiwa na msimamizi wake.

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Wilaya, Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga, 239 Barabara ya Mbambabay, S. L. P 194, 57483 kigonsera – Ruvuma. Simu +255 (025) 2640005, Nukushi +255 (025) 264004, Barua pepe: ded@mbingadc.go.tz, Tovuti: www.mbingadc.go.tz

iii. **MSHAHARA:**
Mshahara wa Kukusanyaji Mapato ni 20% ya makusanyo kwa mwenzi.

IV. MASHARTI KWA UJUMLA

- Mwombaji aambatanishe maelezo binafsi (CV) yenye anuani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini watatu wa kuaminika pamoja na namba zao za simu.
- Maombi yaambatane na nakala za vyeti vya elimu
- Mwombaji aambatanishe cheti cha kuzaliwa.
- Mwisho wa kupokea barua za maombi ni tarehe 14.11.2023 saa 9:30 Alasili.
- Barua zote zitumwe kwa anwani iliyopo hapo chini:-

Mkurugenzi Mtendaji Wilaya,
Halmashauri ya Wilaya Mbinga,
224Barabara ya Mbambabay,
S.L.P. 194,
KIGONSERA, RUVUMA.

NB: Tangazo hili pia linapatikana kwenye tovuti ya Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga ambayo ni:- www.mbingadc.go.tz



Juma Haji Juma
MKURUGENZI MTENDAJI (W)
MBINGA
MKURUGENZI MTENDAJI (W)
HALMASHAURI YA WILAYA
MBINGA

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Wilaya, Halmashuri ya Wilaya ya Mbinga, 239 Barabara ya Mbambabay, S. L. P 194, 57483 kigonsera – Ruvuma. Simu +255 (025) 2640005, Nukushi +255 (025) 264004, Barua pepe: ded@mbingadc.go.tz, Tovuti: www.mbingadc.go.tz